

Swali: Je kazi ya udalali ni dhambi, na Mkristo anaruhusiwa kuifanya?

Jibu: Dalali ni yule mtu anayeza kitu kwa niaba ya mwingine na kisha kuchukua asilimia fulani ya faida ya kile kilichouzwa.

Au pia dalali anaweza kuwa mtu mwenye kutafuta soko la bidhaa ya mtu mwingine na kisha kuchukua asilimia ya faida inayopatikana.

Kama hiyo ndio maana au tafsiri ya udalali, basi mtu akiifanya “SI DHAMBI”, Kwani hata ununuaji wa bidhaa kiwandani na uuzaji masokoni kwa namna moja au nyingine ni “Udalali”, kwani utanunua kwa gharama ndogo na kuuza kwa gharama kubwa na kisha kuichukua ile faida....Hapo tayari umeshakuwa dalali wa wenye kuitengeneza ile bidhaa..

Kwahiyo udalali si dhambi ikiwa tu haujahusisha mambo yafuatayo.

1. UONGO.

Labda umepewa kazi ya kutafuta mteja wa bidhaa husika, halafu ukampata na kumwekea kiwango cha juu sana nje na mapatano na yule aliyekupa bidhaa *(lengo la kufanya hivyo ni ili wewe upate faida kubwa*

na ya haraka)...

Au mteja amehitaji bidhaa au nyumba na wewe ukamlaghai kwa uongo na kumpa kitu ambacho kiko chini ya viwango na huku ukijua kabisa kuwa kitu hiko hakistahili hiyo gharama, Huo wote ni Uongo na udalali huo ni haramu.

2.Dhuluma.(Utapeli).

Unapomdhulumu mtu fedha au bidhaa yake, aidha kwa kumlipa kisasi au kwasababu nyigine yoyote udalali huo ni haramu.

3. Haifanyiki ndani ya nyumba ya Mungu..

Udalali unaofanyika ndani ya Nyumba ya MUNGU ni haramu..

Utaona Bwana YESU aliwafukuza wale madalali wote waliokuwa wanabadili fedha ndani ya nyumba ya MUNGU.

Yohana 2:15 "Akafanya kikoto cha kambaa, akawatoa wote katika hekalu, na kondoo na ng'ombe; akamwaga fedha za wenye kuvunja fedha, akazipindua meza zao;"

Vivyo hivyo kanisani si sehemu ya minada, na udalali, ni sehemu ya Ibada takatifu ya roho na kweli.

Swali lingine je?...Fedha ya udalali inaweza kutolewa sadaka ikiwemo Zaka?.

Jibu ni Ndio!.. kama udalali huo haujahusisha mambo hayo hapo juu, basi inaweza kutolewa sadaka ikiwemo Zaka(*yaani fungu la Kumi*), na ikakubalika mbele za Mungu.

Na je mkristo anaweza kufanya kazi ya udalali??..

Jibu ni Ndio! Anaweza kufanya, ikiwa hatatumia Uongo, au dhuluma, au rushwa, au kufanya ndani ya kanisa la Mungu.

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Je kazi ya udalali ni dhambi?

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

KAMA MHUBIRI USIWE MFANO WA DIOTREFE.

UNAWAFAHAMU MANABII WA UONGO?

TUZIJARIBU HIZI ROHO.

JIHADHARI NA UONGO WA SHETANI UNAOKARIBIANA NA UKWELI.

WALA HAKUSIMAMA MTU PAMOJA NAYE, YUSUFU ALIPOJITAMBULISHA
KWA NDUGUZE

Rudi Nyumbani

Je kazi ya udalali ni dhambi?

Share on:
WhatsApp

Print this post